

# **HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA**



## **SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA (ADA NA UDHIBITI WA UCHIMBAJI WA MADINI YA UJENZI) ZA MWAKA 2017**

(SURA YA. 288 YA 1982)

**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA, (MAMLAKA ZA  
MANISPAA YA MUSOMA ) YA MWAKA 1982**

**SHERIA NDOGO**

Zimetungwa chini ya kifungu Na. 89

**SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA  
(ADA NA UDHIBITI WA UCHIMBAJI WA MADINI YA UJENZI)  
ZA MWAKA 2017**

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Udhibiti wa Uchimbaji wa Madini ya Ujenzi) za Halmashauri ya Manispaa ya Musoma na zitaanza kutumika kuanzia siku zitakapotangazwa kwenye Gazeti la Serikali.
2. Katika Sheria Ndogo hizi:
  - “Afisa Muidhiniwa” maana yake ni mtumishi wa Serikali au mtu yeyote atakayeteuliwa na Mkurugenzi kushughulikia masuala ya udhibiti wa uchimbaji wa madini ya ujenzi katika maeneo ya Halmashauri.
  - “Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Musoma
  - “Madini ya Ujenzi” maana yake ni pamoja na mchanga, mawe, kokoto na udongo (Moram)
  - “Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma
  - “Kuharibu Mazingira” maana yake ni pamoja na kuchimba, kuruhusu kuchimba, kuuza au kununua madini ya ujenzi kutoka katika maeneo yasiyoruhusiwa.
3. (1) Hakuna mtu yeyote atakayechimba au kuuza madini ya ujenzi katika eneo la Manispaa ya Musoma isipokuwa kama anacho kibali kilichotolewa na Manispaa kinachonyesha kuwa eneo hilo limetengwa na kuidhinishwa kwa matumizi ya uchimbaji wa madini ya ujenzi .
  - (2) Kibali cha kuchimba madini ya ujenzi katika maeneo yanayomilikiwa a Halmashauri kitalipiwa
4. Halmashauri itakuwa na uwezo na madaraka ya kufuta au kupendekeza kufutwa kwa kibali chochote kilichotolewa chini ya Sheria Ndogo hizi pale mmiliki wa kibali hicho atakapobainika kuvunja masharti ya kibali au kuvunja Sheria Ndogo hizi.
4. Bila kuathiri masharti ya hapo juu mtu yeyote atakayekuwa na kibali cha kuchimba madini ya ujenzi katika Manispaa ya Musoma atatakiwa kuchimba katika maeneo yaliyobainishwa na Manispaa.

Jina na muda  
wa kuanza

Tafsiri

5. Maeneo ya upatikanaji wa madini ya ujenzi, yatatengwa na Halmashauri kwa kuzingatia Mchoro wa Mipango Miji.
6. Mtu yeyote atakayenunua au kusomba madini ya ujenzi katika Manispaa ya musoma atawajibika kulipia ushuru katika Halmashauri ya Manispaa kulingana na ujazo wa madini ya ujenzi uliosombwa kwa viwango vilivyoainishwa katika jedwali la Sheria Ndogo hizi.
7. Mtu yeyote ambaye atakiuka Sheria Ndogo hizi au kwa namna yoyote ile atamsaidia mtu yeyote kukiuka Sheria Ndogo hizi au kuzuia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atahukumiwa kifungo cha miezi kumi na mbili jela au faini isiyopungua kiasi cha shilingi laki mbili na kisichozidi shilingi milioni moja au vyote kwa pamoja kifungo na faini.
8. Mkurugenzi pale atakapokuwa ameridhika kuwa mtu yoyote ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi anaweza kumtoza mtu huyo faini isiyozidi ile iliyowekwa na Sheria Ndogo hizi endapo mtu huyo atakiri kuwa kutenda kosa hilo.

Adhabu

---

**JEDWALI A**

<i>Ujazo wa mchanga , Kokoto ,moramu na mawe</i>	<i>Ushuru (Tshs )</i>
<b>MCHANGA</b>	
Lori lenye tani 1 – 5.....	3,000/= kwa kila tripu
Lori lenye tani 5 – 8.....	5,000/= kwa kila tripu
Lori lenye tani 10 – 15.....	7,000/= kwa kila tripu
Lori lenye tani 15 kuendelea.....	8,000/=kwa kila tripu
<b>KOKOTO</b>	
Lori lenye tani 1 – 5.....	4,000/= kwa kila tripu
Lori lenye tani 5 – 8.....	6,000/= kwa kila tripu
Lori lenye tani 10 – 15.....	7,000/= kwa kila tripu
Lori lenye tani 15 kuendelea.....	10,000/=kwa kila tripu
<b>MAWE</b>	
Lori lenye tani 1 – 5.....	3,000/= kwa kila tripu
Lori lenye tani 5 – 8.....	5,000/= kwa kila tripu
Lori lenye tani 10 – 15.....	7,000/= kwa kila tripu
Lori lenye tani 15 kuendelea.....	8,000/=kwa kila tripu

Nembo ya Halmashauri ya Manispaa imebandikwa kwenye sheria ndogo hizi kufuata azimio lililopitishwa katika kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kilichofanyika tarehe .....mwezi .....2017 mbele ya:

.....  
**MH: PATRICK WILLIUM GUMBO  
MSTAHIKI MEYA  
HALMASHAURI YA MANISPAA  
MUSOMA**

.....  
**FIDELICA G. MYOVELLA  
MKURUGENZI  
HALMASHAURI YA MANISPAA MUSOMA**

NAKUBALI,

**TAREHE** .....  
**DODOMA**

.....  
**GEORGE B. SIMBACHAWENE(MB)  
WAZIRI WA NCHI – OR - TAMISEMI**

---